

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S. L.P 1055, ARUSHA
Simu : (027) 2503538/ 2507928
Nukushi: (027) 2505973
Barua pepe: rbcarusha@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

DESEMBA 04, 2020

WANNE WAHUKUMIWA KWA KUGHUSHI VYETI VYA ELIMU

Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Arusha inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na. 11/2007 ambapo moja wapo wa jukumu kuu la TAKUKURU kwa mujibu wa sheria hiyo ni jukumu la uchunguzi na mashtaka.

Tunapenda kuarifu umma kwamba katika kipindi cha mwezi Novemba na Desemba 2020, TAKUKURU Mkoa wa Arusha imeshinda kesi tano, nne kati yake zikiwahusisha watumishi wanne wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli walioghushi vyeti vya elimu na kufanikiwa kupata kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Kesi hizo zilizokuwa zikiendeshwa katika mahakama mbalimbali mkoani Arusha, zimekamiliwa na hukumu kutolewa kwa wote waliokutwa na hatia. Mchanganuo wa kesi hizo ni kama ifuatavyo:-

1. CC. Na. 28/2019; Kesi hii ilimhusu LEMALI GOIGOI KIPUYO aliyekuwa afisa mtendaji wa kijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Mnamo tarehe 03.12.2020 Mahakama ya Wilaya ya Monduli ilimtia hatiani mtuhumiwa kwa kosa la kuwasilisha cheti cha uongo cha Maendeleo ya Jamii kilichomwezesha kupata ajira kwa aliyekuwa mwajiri wake ambaye ni Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Kinyume na kifungu cha 342 cha sheria ya Sheria ya Kanuni za Adhabu (Penal Code) Sura ya 16.
Mshitakiwa alihukumiwa kifungu cha nje na kutakiwa kutorudia makosa ya aina hiyo ndani ya mwaka.

2. CC.18/2019; Kesi hii ilimhusu NYANGUSI SIRIAM SIVITE aliyekuwa afisa mtendaji wa kijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Mnamo tarehe 03.12.2020 Mahakama ya Wilaya ya Monduli ilimtia hatiani mshtakiwa kwa kosa la kuwasilisha cheti cha uongo cha Maendeleo ya Jamii kilichomwezesha kupata ajira kwa aliyekuwa mwajiri wake halmashauri ya Wilaya ya Monduli, kinyume na kifungu cha 342 cha sheria ya Sheria ya Kanuni za Adhabu (Penol Code) Sura ya 16.
Mshitakiwa alihukumiwa kwenda jela mwaka mmoja au kulipa faini ya Shilingi Laki mbili (Sh. 200,000/-). Mshitakiwa alilipa faini na kuachiwa.
3. CC.17/2019; Kesi hii ilimhusu SAIBUL SUPAK TING'IDE aliyekuwa afisa mtendaji wa kijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Mnamo tarehe 03.12.2020 Mahakama ya Wilaya ya Monduli ilimtia hatiani mshtakiwa kwa kosa la kuwasilisha cheti cha uongo cha Maendeleo ya Jamii kilichomwezesha kupata ajira kwa aliyekuwa mwajiri wake Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, kinyume na kifungu cha 342 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu (Penol Code) Sura ya 16.
Mshitakiwa alihukumiwa kwenda jela mwaka mmoja au kulipa faini ya Shilingi Laki mbili (Sh. 200,000/-). Mshitakiwa alilipa faini na kuachiwa.
4. CC.19/2019; Kesi hii ilimhusu NASIRA KUYA KISIMIRI aliyekuwa afisa mtendaji wa kijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Mnamo tarehe 03.12.2020 Mahakama ya wilaya ya Monduli ilimtia hatiani mshtakiwa kwa kosa la kuwasilisha cheti cha uongo cha Maendeleo ya Jamii kilichomwezesha kupata ajira kwa liyekuwa mwajiri wake Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, kinyume na kifungu cha 342 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu (Penol Code).
Mshitakiwa alihukumiwa kwenda jela mwaka mmoja au kulipa faini ya Sh. Laki mbili (Sh. 200,000/-). Mshitakiwa alilipa faini na kuachiwa.
5. CC. Na. 122/2020; Kesi hii ilimuhusu PROSPER RAPHAEL KIRIA aliyekuwa mwajiriwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kwa nafasi ya Mhasibu. Mnamo tarehe 23.11.2020 Mahakama ya Wilaya ya Karatu ilimkuta na hatia mshtakiwa kwa kukiuka kifungu cha 22 cha PCCA na vifungu vya 258 na 270 vya Sheria ya Kanuni za Adhabu (Penol Code) Sura ya 16.
Mshitakiwa amehukumiwa kulipa faini ya Sh. 2,070,000/- au kwenda jela miaka miliwili na pia kurejesha fedha alizoiibia Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kiasi cha Sh. 2,038,044/-.
Mshitakiwa alilipa faini na kutakiwa kurejesha fedha alizoiiba.

Katika tukio lingine mnamo tarehe 20.11.2020, ofisi ya TAKUKURU wilaya ya Longido ilimfikisha mahakamani LIDYA SULULU MOLLEL kwa kosa la kutoa

taarifa/ ushahidi wa uongo mahakamani kinyume na vifungu vya 102 na 104 vya Sheria ya Kanuni za Adhabu (Penal Code) Sura ya 16. Mshitakiwa alifikishwa mahakama ya wilaya ya Longido na kufunguliwa kesi CC. Na. 106/2020.

Awali katika uchunguzi uliokuwa unafanywa na TAKUKURU Wilaya ya Longido, mshitakiwa alichukuliwa maelezo kama shahidi katika kesi CC. Na 19/2020, lakini alipofikishwa mahakamani kutoa ushahidi kama alivyokuwa amaeleza hapo awali, alikana maelezo yake ndipo alipokamatwa na TAKUKURU na kushtakiwa kwa kosa la kutoa maelezo ya uongo.

Tunawaasa wananchi kuwa waaminifu na kuzingatia Sheria, Kanuni, na Taratibu wanapohitaji huduma mbalimbali katika taasisi za umma au binafsi ili kuepuka kujihusisha na vitendo ambavyo vinaweza kuwasababisha kuchukulia hatua za kisheria.

Imetolewa na:

SABAS SALEHE

Kny: MKUU WA TAKUKURU (M) ARUSHA

